MAKALA

Wanaitazama Tanzania yetu kwa jicho la husda

na margwe cyril miontini

KWA mara ya kwanza naomba nitumie haki yangu ya kikatiba kutoa maoni kwenye gazeti lililotukuka kwa kuandika habari za uchambuzi bila kusitasita wala kurudi nyuma.

Novemba 30, 1999 marais wa Tanzania, Kenya na Uganda walisaini mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (sijui kama kulikuwa na maoni ya wananchi yaliyoombwa). Miaka mitano baadaye, yaani Januari 2005, utaratibu wa ushuru wa pamoja (custom union) ulianzishwa ukiaminika ni hatua ya msingi kabla ya soko la pamoja, sarafu moja na mwishoni Shirikisho.

Nimesikia tunatakiwa kutoa maoni kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki ambalo linasemekana litakuwa tayari ifikapo mwaka 2013. Nafikiri na kujiuliza kama kutoka hatua moja kwenda nyingine, yaani Jumuiya hadi ushuru wa pamoja tumetumia karibu miaka mitano, inawezekanaje kwa miaka minane iliyobaki hatua zote ziwe zimefuatwa na tuwe tumefika kwenye Shirikisho?

Tunakimbizwa haraka kwenye Shirikisho kwa maslahi ya nani? Naona kuwa na sarafu moja kama hatua ya kuelekea Shirikisho kabla ya 2013 ni ndoto, tena ya mchana kweupe! Au shirikisho kwanza halafu mchakato baadaye?

Ni kweli kuna nia ya dhati ya kutushirikisha wananchi? Mimi naona limekuja baada ya mkutano wa dharura wa wakuu uliofanyika Dar es Salaam Mei 30, 2005, ambao katika mengine waliona ni muhimu kushirikisha wananchi, naomba ninukuu, imeandikwa Kiingereza (wapo wanaoita kitaalam): They further observed that a strong federation is only possible if it is owned by the people of East Africa themselves through the effective and informed participation from the very beginning of the process through to the very end' (The state of East African Report 2006, pg 7). Nafikiri hali halisi imelazimisha uwapo wa ushikishwaji wa wananchi, vinginevyo wananchi wanaweza kuona Shirikisho kama la viongozi tu.

Siafiki uhusiano wowote wa nchi yangu na nyingine ambayo naona hamna uwiano sawa wa kimaslahi, vinginevyo iwe kwa mambo ambayo si ya kawaida, mfano maafa na vita ya ukombozi. Nina hoja zangu chache ambazo naamini zina uzito wa kutosha kama zitafikiriwa vizuri. Kwa kuangalia suala zima la elimu katika eneo la Afrika Mashariki, ukweli unaonyesha kwamba Kenya ni nchi inayoongoza kwa idadi kubwa ya wasomi. Nafikiri mfumo wake wa elimu kwa watu wake unaweza kuwa sababu, nafikiri sisi bado tunahitaji kufanya mageuzi ya kizalendo katika uwezeshaji wa watu wetu hasa katika elimu ya juu.

Mfano, wakati Tanzania tuna uwiano wa madaktari wa 2: 100,000, wenzetu Kenya wana uwiano wa 13:100000 (The state of East Afican Report 2006 pg 47). Kwa tafsiri rahisi, ni kwamba idadi ya madaktari Kenya ni karibu mara sita ya idadi ya madaktari wetu. Huu ni mfano wa sehemu tu ya hali halisi, achilia mbali taaluma nyingine.

Kwa hali hii wataachaje kuajiriana wenyewe kwenye nafasi ambazo si za mzunguko wakati wenyewe ndio wenye idadi kubwa ya wasomi? Na kuna madai kwamba baadhi yao wana mizizi mirefu ya ukabila! Hapo bado wapo watu wa kwetu wanaotaka kuharakisha kufunguliwa kwa soko la ajira la Afrika Mashariki!

Nashindwa kuelewa wanaotaka kufungua soko hilo wanataka kuwafungulia kina nani? Siamini kama wanaotuambia tusiogope wanamaanisha wanachokiongea.

Mimi naona kuna kila sababu ya kufikiri kizalendo kabla ya kufanya uamuzi wenye athari za muda mrefu. Kama ni mimi leo, mawazo tu ya kufungua soko la ajira la kwenye serikali zaAfrika Mashariki ningeyapiga marufuku hata kujadiliwa mpaka tutakapokuwa na uwiano wa wasomi kwa nchi zetu, walau unaokaribiana sana kama si sawa kabisa, naamini inawezekana kusubiri tukawa sawa ndio tukaungana.

Pamoja na idadi ndogo ya wasomi tulionao, bado ajira ni tatizo sugu ndio maana wakati wa kampeni ni moja kati ya masuala yaliyochukua uzito wa juu na tuliahidiwa kujengewa mazingira ya upatikanaji wa ajira. Naamini soko hilo likifunguliwa ile nafasi nyembamba ya upatikanaji wa ajira tuliyoahidiwa kujengewa mazingira yake itakondeshwa zaidi na hatimaye kubaki kuwa ajenda kwa kampeni za 2010.

Suala la uwakilishi pasa katika Bunge la Afrika Mashariki, naliona kama linaweza kuleta hatari kubwa ya watu wachache (mfano Rwanda – milioni 9) kuwafanyia uamuzi watu milioni 40! Hilo linawezekana kama idadi ya wabunge ni sawa kwa kila nchi. Athari ya hili ni kubwa na sitaki kwenda mbali kulielezea. Najua wapo watakaopinga kwa vigezo vingine vingi tu, lakini ukweli unabaki pale pale, kwamba tunaweza kufanyiwa uamuzi na watu wachache.



Mwalimu Nyerere

Kwa kuangalia suala zima la ardhi, takwimu zinaonyesha kwamba Rwanda ina watu 293 kwa kilometa moja ya mraba, kiasi ambacho ni moja kati ya vikubwa duniani. Tanzania ina idadi ndogo kabisa katika Afrika Mashariki – ya watu 37 kwa kilometa moja ya mraba wakati Uganda na Kenya zina watu 53 na 93 kwa kilometa ya moja ya mraba, kwa mtiririko huo (the State of East African Report 2006 pg 15).

Tayari takwimu hizi zimeonyesha shida ya ardhi iliyopo Rwanda, na rasilimali ya ardhi tuliyonayo sisi inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha wao kutaka mchakato uharakishwe.

Kwa hali halisi ni kwamba tunatofautiana sera za ardhi, sisi tunapata kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya Mwalimu Nyerere (kuna minong'ono kwamba wapo ambao hilo la Kambarage linawapa shida kulitamka) kwa kutujengea sera ambayo nafikiri ni nzuri kuliko za wenzetu.

Wenzetu wa Kenya walitumia mfumo wa ulowezi ambao uliwaacha wengi bila ardhi yenye rutuba. Nafikiri hatuwezi, kama ardhi tuliyonayo ni hazina, mpaka itakapoingia kwenye mikono ya wageni kwa vigezo vya Shirikisho ka utandawazi. Sisemi wasipewe ardhi, ila nasisitiza kwamba utararibu wetu ufuatwe hapa kwetu (labda miaka 50 ijayo tutakuwa tayari kama kuna mikakati madhubuti ya kutuandaa). Suala la kwamba kuna watu wanaoitazama Jamhuri yetu kwa jicho la husda kwa sababu zao binafsi na wanatafuta mwanya wowote wautumie.

Suala la Rais Yoweri Museveni wa kuzungumza hadharani kwamba urais wa Shirikisho unamfaa yeye kwanza ni la kufuatiliwa kidogo si la kuachiwa hivi hivi... ni hatari kuliacha! Ni nani kamhakikishia kwamba wananchi watakubali Shirikisho?

Ni nani nyuma ya pazia anamhakikishia kwamba atakuwa rais wa Shirikisho? Mimi binafsi siamini kama tunahitaji kupata msaada wa Scotland Yard kuhisi tu kwanuba kuna nguvu nyuma ya Museveni! Nafikiri watu hawakumbuki kirahisi kwamba mambo ya kubadili Katiba hapa Tanzania hayajawahi kufikirika kwa wananchi, na kwa mantiki hiyo suala la yeye kubadili Katiba ya Uganda bado lipo kama mshangao kwenye vichwa vya Watanzania.

Suala la kuonyesha kutaka urais wa Shirikisho la Afrika Mashariki ambalo bado halijaundwa na wananchi kama litakuwapo au la, nafikiri ni dalili kwamba akipata anaweza kutumia uzoefu wake kubakia! Na sisi tukaambiwa wale wanaojiita wahisani au wafadhili (ambao miaka ya nyuma waliwahi kuitwa majina kama mabeberu, wakoloni, wanyonyaji na mengine mengi tu ya aina hiyo) ndio wametuamulia iwe hivyo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Tanzania alipoulizwa kama Serikali itafuata maoni ya wananchi hata kama yataonekana kutokukubaliana na Shirikisho alisita kusema ndio au hapana. Kwa nini waziri amesita kusema ndio au hapana kuhusu kufuatwa kwa maoni yetu?

Umefika wakati, watu wote tunaoona tunahitaji muda wa kutosha, mipango thabiti na endelevu ya kujiandaa, tuungane kuangalia utaratibu wa kufanya 'counter check movement against fast tracking' mapema kabla fast trucking haijafanya kazi fasti.

Vingenevyo kutokujua kwetu kunaweza kutumika kama baraka. Wenzetu wanajua wanataka kupata nini na wanataka zoezi hilo liharikishwe ili wapate haraka wanachokitaka kabla sisi hatujashtuka, ili tukishtuka tukute wameshapata na sisi tumepoteza walichopata wenzetu.

Kwa mujibu wa jarida la The East African Lawyer la Oktoba 2005 (toleo la 8 uk. 31) Shirikisho litakuwa na uwezo wa mambo saba ambayo yanaonekana ni ya msingi kabisa, la kwanza likiwa ni ulinzi wa Shirikisho na maelezo yanaendelea kwamba kutakuwa na jeshi la Shirikisho (East African Defence Force).

Kwa ukubwa wa jeshi katika Afrika Mashariki, nchi ndogo kabisa za Rwanda na Uganda ndizo zenye jeshi kubwa (The East African Report2006 uk. 11). Sababu ziko wazi, likiwamo la LRA (Lord's Resistance Army) kuhakikisha Uganda ina jeshi kubwa, na ni wazi kwamba Uganda ingependelea mchakato uharakishwe (na Museveni awe Rais) ili lipunguze gharama za uendeshaji wa jeshi na ikiwezekana litumike kuwafutilia mbali LRA.

Kwa mtiririko huo, kuna uwezekano wa watu kubebeshwa mizigo isiyotuhusu. La kujiuliza ni kwamba hivi ni kweli sisi tunataka kuwahi kubebeshwa mizigo ya watu wengine wakati tuna yetu mingi na mizito? Naonelea ni vizuri ikiundwa kamati huru ya kutatua migogoro Afrika Mashariki ambayo haitakuwa na majukumu mengine, na wanaoiunda wasiwe wanasiasa. Imalize kwa diplomasia migogoro kabla ya Shirikisho. Baada ya kuwa shwari ndio tuangalie kama tunaweza kuungana katika mambo ambayo kila nchi inafaidi kwa uwiano sawa na yasiyo na uelekeo wala fikra za hila na kutumiana.

Tanzania inashikilia asilimia 72 ya maeneo ya hifadhi (Kenya 18%, Uganda 9% na Rwanda 1%). Kwa tafsiri rahisi ni kwamba sisi ndio wenye hifadhi karibu zote. Tujiulize katika Afrika Mashariki uwiano wa kipato cha soko la utalii linafanana na tulivyo navyo?

Kama hakuna, je, wapo wanaohusika na hujuma za kuhakikisha hatufaidi na tunataka kuungana nao? Achilia mbali kunadiwa kwa mda mrefu kwamba Mlima Kilimanjaro upo Kenya, kuna minong'ono kwamba hata sasa wapo wanaonadi kwamba sasa Serengeti haipo Tanzania.

Nahisi hili nikiita uhuni nitakuwa sijapungukiwa na maadili. Ni kweli, hata sisi tunatangaza sana vivutio vyetu lakini sidhani kama kuna Mtanzania amewahi kutangaza maeneo ya watu wengine kama ni yetu. Kama huu uhuni hauna uungwaji mkono ndani, mbona hamna anayejitokeza kutoka Kenya kuwapinga wanaohubiri hivyo? Hapo tupo kwenye Jumuiya bado Shirikisho!

0754535637
margwe12@yahoo.co.uk